RAIS Moi akihudhuria misa katika Kanisa la St. Barnabas Church, mjini Nairobi Jumapili iliyopita. PICHA: K.N.A.

Ibada ya Hijja, fadhila na sharti zake kwa iwe ni Faida kwa Wahijaji wote

Na Sheikh Nassor Khamis

HIJA ni nguzo (sharti) ya tano katika nguzo ya Uislamu na maana yake hasa hii hija au kuhiji ni kuikusudia nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu yani Alkaba iliyoko huko Makka ili kwenda kutekeleza vitendo maalumu vya: kutufu, kutembea baina ya Safa na Marwa, kusimama huko Arafa kumuomba Mwenyezi Mungu na mengine mwengi.

Nayo hija yamlazimu tu yule mwenye uwezo wa kugharimia safari ya kwenda huko Makka, nayo ni lazima tu katika umri wa mtu mara moja. Na Mtume wetu Muhammed S.A.W. alihiji mara moja katika mwaka ule alioifariki, na ndiyo mana hija yake ikaitwa "Hija ya Kuaga", kwa sababu hakuna hija ambayo Mtume Muhamed S.A.W. alikutana na idadi kubwa sana ya Waislamu kuliko hija ile.

Na katika maneno yake mashuhuri aliyosema siku ile ni pamoja hii, "Jifunzeni mambo ya ibada yenu kutoka kwangu, huenda nisikutane nanyi baada ya mwaka huu! Na yakika maneno hayo yalikuwa ni ya kweli kwani baada ya miezi mitatu ya Hija hiyo, Mtume S.A.W. alifariki dunia.

FADHILA ZA HIJA

Kuna hadithi nyingi za Mtume S.A.W. zinazothibitisha fadhila za hija na malipo yake mema na mimi nitataja tu baadhi ya hadithi hizo za, mafundisho hayo ya Mtume wetu.

- **Wakati moja aliulizwa Mtume S.A.W. ni amali gani iliyobora? Mtume akajibu kuwa ni Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Akaulizwa kisha nini? Mtume akajibu kuwa ni Hija iliyofanywa vizuri. Bukhari**
- **Amesema Mtume S.A.W. kuwa mwenyekuhiji na asifanye maovu kama kuundama, wala asiseme machafu yatafutika madhambi yake awe safi sawa na ile siku alozaliwa na mamake (Bukhari na Muslim)**
- **Amesema mtume S.A.W. Jihadi ya mtu mzima na aliye mnyonge wa hali na mwanamke ni Hija na Umra. Annasai**
- **Amesema Bibi Aisha Ra, "Nilimwuliza Mtume AS, jee inawapasa wanawake kupigana jihadi? Akasema Mtume AS, inawalazimu wao jihadi isiyokuwa na mapigano. Hija na Umra. Bukhari.**

Hizo ni baadhi tu ya hadithi za Mtume zinazotufahamisha fadhla na malipo mema kwa mwenye kuitekelaza nguzo ya Hija.

UZINDUSHO

Ni lazima kwa yule mwenye kutaka kwenda hija awe na uwezo wa kiafya na mali, yaani awe mzima na awe na fedha za kumtosha yeye safarini huko na za kuwaatia watu wake mpaka atakaporudi. Na akiwa yule atakayekwenda hija yuadaiwa au hajatoa zaka za mali yake na akawa akililipa deni hilo au akitoa zaka hizo zitakazosalia hazitamtosha kwa safari yake ya Hija, basi hija hiyo haitamlazimu mtu huyo. Haya yakiwa na maana kwamba kutoa zaka ni lazima kutangulizwe kuliko Kuhiji. Na akiwa mtu yuwadaiwa na akawa yule anayedai ataka pesa zake, basi deni litagulizwe kuliko Kuhiji. (Itaendelea)

HUYU ni Ustadh Abubaker Abdulrahman ambaye kila Alhamisi na Juma kuanza saa kumi hadi saa kumi ba mbili huwa akitoa mawaidha ya Kiislamu Majengo Sokoti. PICHA: ABEID KARAMA

MWENYEKITI wa East African Powet and Lighting Company Bw. J. K. Gecau alipomtembelea Mkuu wa Pwani Bw. Luka Galgalo katika afisi yake akiwa pamoja na Meneja wa Pwani Bw. Lawrence Keitany. PICHA: NATIONAL STUDIO

AKINAMAMA WA KIISLAMU WANATOA WAADHI

ISLAMU WAKANYWA hata katika vitabu vidogodogo kama hidayatul atfal kujishabihisha na makafiri katika mambo yasiyokhusika nao (yaani ambayo hakuna afanyae illa wao) kwa sababu ya neno lake mtume S.A.W. alilosema; "Mwenye kujishabishisha na watu basi nae huwa katika wao". Hivi ni kusema kwamba mwenye kujishabihisha na Islamu huwa miongoni mwa Islamu na mwenye kujishabihisha na makafiri huwa miongoni mwa makafiri.

Haya ni katika mambo ya kilimwengu, je iwapo kujishabihisha huko ni katika mambo ya dini? Bila shaka ubaya wake ni mkubwa zaidi.

Mambo yafanyikayo katika kupamba maarusi kwa vao na mila ya kinasara yana ukhusiyano fulani na ukristo. Ndipo wao wenyewe wakawa huzieka na kuzihifadhi nguo zile apambiwazo mwanamke katika harusi siku ya kufa akapabwa kwa nguo hizo.

Kabla ya kuja adhana (Mwadhini) Mtume S.A.W. alikuwa akitafuta ndio ya kuwakusanya Islamu wakti wa sala. Akapawa shauri kupiga kengele, akasema: "La, hayo ni ya manasara". Akapawa shauri la kupiga barugumu, akasema: "La, hayo ni ya mayahudi". Akapawa shauri kukoka moto ili kila atakaeona muanga wake ujuwe kuwa wakati wa sala umefika, akasema: "La, hilo ni la majusi". Ndipo baadhiya masahaba walipo oteshwa adhana hii tuijuayo ambayo haikushabihishana na watu wa dini nyengine.

Na kama tujuvyo kuna Nyakati Maalumu ambazo Islamu wakatazwa kuswali katika nyakati hizo, kama mwanzo wa kutoka jua na kabla ya kumalizika kutwa jua, kwa sababu ya kutahadhari na kuchelea na kujishabihisha na makafiri ambao hufanya ibada zao katika nyakati hizo.

Haifai kabisa kupima maovu kipimo cha "lipo lililo ovu zaidi" Dogo huweza kuleta madhara makubwa ambayo hayakutarajiwa dhambi zake zikawa kubwa kuliko lile lionekanalo kuwa ni kubwa. Na ovu dogo haliitwi dogo illa iwapo mtu limempitia mara moja kwa kupigwa kumbo za shetani.

Lakini mwenye kudumu na kuendeleya kufanya ovu lolote hata ikawa dogo namna gani, hukumu yake katika sharia ni kama afanyae kubwa.

CEASAR C. MADDANGANHA

Mwandishi mashuhuri Ceasar Charles Maddanganha hivi sasa yuko mbioni kuwasilisha vitabu vyake viwili vya Kiswahili kwa wanafunzi wa upili ambavyo vinaelimisha juu ya ufupishaji wa lugha ya Kiswahili kwa waalimu na wanafunzi. Bw. Ceasar hivi sasa yuko katika harakati za kuandika kitabu cha Riwaya ambacho kinategemewa kinategemena kuwasisimua wasomaji wa vitabu vya hadithi vya Kiswahili nchini.

RAIS Moi akiongoza Harambee ya kusaidia hospitali ya kathiani katika iveti kaskazini huko wilaya ya machako. Hapo anapokea mchango wa Jemedari Mulinge. PICHA: K.N.A.

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO.

SWAHILI CROSSWORD NO 147



KWENDA KULIA:

1. Mala ni mlaleo mla jano . . .
5. Wingi wa yeye
6. Cha moto
7. Kulalia kwa kuku juu ya mayai
9. Ama
10. Chombo cha bahari
12. Watetea . . . mgomba si wao
14. Aina ya ndege
15. Kiungo cha maneno
16. Zidisha

KWEDA CHINI:

1. . . . kinguoni mwako _
2. Shabaha
3. Mwenda tezi na omo maregeo . . .
4. Huvaliwa shingoni
5. Hunukia linapochanua
8. Tamko la kukataa
11. Mwenziwe mshale
12. Ufupi wa "Na wao"
13. Jitu zima
15. West Africa.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 145

1. Paschal Chagembe, Sanduku La Posta 84968, Mombasa
2. Abudi Bwanaidi, Sanduku La Posta Mwikaa Mtenzi 81543 MOMBASA.
3. Abbasi Shaffi Sanduku la Posta 87922, Mombasa

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK.*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 146 —

KWENDA KULIA:

1. MWAVULI, 6. NENEA, 8. IRINGA, 9. TEO, 10. MKAUMA 13. TAMBAA, 16. JE, 17. UA, 18. KIZIMBA.

KWENDA CHINI:

2. WARAKA, 3. UNGAMA, 4. LEA, 5. IN, 7. ELEKA, 11. UTESI, 12. AMALI, 14. AULA, 15. ZUA.

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:-

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za Fumbo hili lipekelwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270, Mombasa Kenya. Siku ya Jumatano tarehe September 22, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.